# Handeni Yetu

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. April- June 2017 Toleo Namba 04

HUTOLEWA KILA BAADA YA MIEZI MITATU



Shule 11 zapongezwa kilele cha juma la Elimu uk 9

Wananchi wahimizwa kupeleka watoto chanjo Uk 5



Habari Katika Picha Uk 12



## Halmashauri ya Wilaya ya Handeni yawataka Viongozi wa ngazi ya chini kushiriki kukusanya mapatoUK3



Viongozi Mbalimbali ngazi ya Jimbo wakiwa kwenye Baraza lililofanyika June katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Handeni kujadili masula mbalimbali ikiwemo namna ya kuboresha ukusanyaji wa mapato.

## YALIYOMO NDANI

Wafanyakazi Wilayani Handeni waungana na wafanyakazi Duniani kuadhimisha siku yao.UK4




Duka la kuhifadhi dawa lafunguliwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Handeni UK7



**Waheshimiwa Madiwani na wakuu wa Idara na Vitengo wafanyiwa semina ya Uelewa wa pamoja kuhusu fedha za Ruzuku**



Jukwaa la kuwawezesha wanawake kiuchumi lazinduliwa Wilayani Handeni Uk 6



Halmashauri ya Wilaya ya Handeni yapokea miche 4000 ya mbegu za Korosho UK12



# TAHARIRI

*Karibu mpenzi msomaji wa Jarida la Handeni yetu awamu ya 4 ambapo lengo la jarida letu ni kuwahabarisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu ili liwe nyenzo na daraja la kukuza maendeleo katika Halmashauri . Lengo la Halmashauri ni kuhakikisha kuwa Jarida la Handeni Yetu linapatikana katika kila Ofisi ya Kijiji na Kata ili kuwapa wananchi nafasi ya kusoma na kuelewa namna Halmashauri inavyotekeleza shughuli zake.*

*Aidha tunakaribisha habari na makala mbalimbali kutoka kwenye vijiji na Kata. Makala hizo zinaweza kuelezea jinsi utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo zinavyofanyika katika kijiji au kata husika.*

*Asanteni na tunawatakia usomaji mwema.*




# YALIYOMO

Mkurugenzi Mtendaji ashukuru msaada wa kompyuta 2 kutoka BAYPORT Uk8




Mbunge Handeni vijijini afanya ziara ya kutembelea miradi ya mfuko wa Jimbo uk6




Miradi ya Malambo ya ajira za muda TASAF zapongezwa na Baraza la MadiwaniUK10



Vikundi 5 vya wajasiliamli vyawakilisha Handeni maonesho ya Biashara Mkoani Tanga.Uk3

Handeni yapongeza jamii ya wamasai kwa kukomesha vitendo vya ukeketaji UK13

Shughuli za kibinadamu marufuku mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji UK11








## LINATOLEWA NA:

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.
S.L.P 355
Handeni, Tanga
Email:ded@handenidc.go.tz
Tovuti: www.handenidc.go.tz
fcebook: handenidc

*DIRA(VISION)*

*Kuwa na jamii iliyoelimika na kuwa na maisha bora.*

*DHAMIRA (MISSION)*

*Kuipatia jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni maisha bora kiuchumi kwa kutumia vizuri rasilimali zilizopo kwa kudumisha Utawala Bora ili kuboresha maisha ya jamii*

## Halmashauri ya Wilaya ya Handeni yawataka Viongozi wa ngazi ya chini kushiriki kukusanya mapato

Handeni yataka ushirikishwaji viongozi ngazi za chini katika kupanga na kukusanaya mapato ya Halmashauri ili kuwahudumia vizuri wananchi.

Agizo hilo lilitolewa na mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Handeni, Mh.Ramadhani Diliwa katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya wilaya ya Handeni .

Diliwa alielekeza kuwepo kwa umakini katika kusaidiana katika ukusanyaji wa mapato ya halmashauri. Alishauri kuwepo kwa ushirikiano baina ya madiwani na viongozi wa Kata katika kupanga na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali. Aliwataka kuhoji kwa kina na kuwabana wakusanyaji ili kutoruhusu mianya ya upotevu wa mapato ya serikali katika Halmashauri .

Katika kuhamasisha ukusanyaji wa mapato ya serikali, Mwenyekiti wa Halmashauri alielekeza uandaliwe utaratibu wa kutoa motisha kwa Kata zitakazofanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya serikali. Aidha, aliwataka watendaji kutosingizia upungufu wa mashine za kieletroniki (EFD) za kukusanya mapato kama ni sababu ya kukusanya mapato chini ya kiwango. *"Hakikisheni mnasimamia vizuri vitabu vya risiti halali vinavyotumika kukusanya mapato na viwe vinawasilishwa kwa wakati Halmashauri kwa ajili ya ukaguzi"* alisisitiza Diliwa

Akichangia katika kikao hicho, Diwani wa Kata ya Kang'ata, Abraham Mollel alihoji utaratibu wa madiwani kulalamikia ubadhirifu wa mapato uliofanyika katika Kata zao. Alisema "si jambo jema kwa madiwani kulalamikia mapungufu na ubadhirifu wa mapato uliofanyika katika Kata zao, madiwani wana wajibu wa kusimamia vizuri mapato ya serikali katika Kata na kufahamu kiasi kilichokusanywa na kuwasilishwa makao makuu" alisisitiza Mollel.

Akijibu baadhi ya hoja, Katibu wa Baraza la Madiwani ambaye pia ni Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Handeni, Bw.William Makufwe alisema kuwa pamoja na ukweli kuwa mashine za kieletroniki za kukusanyia mapato ni gharama, Halmashauri imekwisha nunua mashine za kukusanyia mapato 30 na imejipanga kwenye bajeti ijayo kuongeza mashine nyinyine 50 ili kukamilisha mahitaji ya mashine 80 kwa Halmashauri.

Aliwataka watendaji kuwa waadilifu katika kutekeleza majukumu yao hasa katika kukusanya mapato ya serikali ngazi ya Kata.

"Tukijikita katika uadilifu kwa watumishi na viongozi pamoja na upungufu wa mashine za kukusanyia mapato bado vitabu vilivyopo vitaiwezesha Halmashauri kukusanya mapato kulingana na malengo iliyojiwekea" alisisitiza Makufwe.

Mkurugenzi alilitaarifu Baraza la Madiwani kuwa Halmashauri imepanga kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuwa na sura mpya. Aliongeza kuwa watendaji wa vijiji watakaofanya vizuri watajaza nafasi za watendaji wa Kata watakaofanya vibaya katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, amesisitza kuwa Kata itakayofanya vizuri katika ukusanyaji mapato itapewa motisha.

## Vikundi 5 vya wajasiliamali vyawakilisha Halmashauri ya Wilaya Handeni kwenye maonesho ya Biashara Mkoani Tanga.

Vikundi vitano vya biashara viliwakilisha Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kwenye maonesho ya biashara TANTRADE yaliyofanyika mkoani Tanga.

Lengo la maonesho hayo lilikuwa ni kuzitangaza fursa za viwanda, biashara na uwekezaji zinazopatikana mkoani Tanga Katika kuijenga Tanzania ya Viwanda.

Pili ni kujengea uwezo wajasiliamali waliopo mkoani Tanga Katika kutafuta masoko na kuzitangaza bidhaa zao.

Halmashauri zote 11 za mkoa wa Tanga, Taasisi za serikali, Viwanda vyote vilivyopo Tanga vilishiriki.

Maonesho hayo Yalianza Tarehe 28/5 hadi 6/6 2017 na vikundi vilivyowakilisha Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ni pamoja na Mkaliatabu cha Kata ya Kitumbi, Jumukulu cha Kata ya Mkata, Jiongeze cha Kata ya Mazingara, Balalu cha Kata ya Misima na Uwamta cha Kata ya Mkata.



# Wafanyakazi Wilayani Handeni waungana na wafanyakazi wengine Duniani kuadhimisha siku ya Wafanyakazi.



*Wafanyakazi wa Handeni wakiwa kwenye maandamano ya pamoja.*

Wafanyakazi Wilayani Handeni wameungana na wafanyakazi wengine duniani katika kuadhimisha maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani iliyofanyika Kiwilaya kwenye Viwanja vya Chanika vilivyopo Wilayani Handeni.

Maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya " Uchumi wa Viwanda uzingatie kulinda Haki, Maslahi na Heshima ya Wafanyakazi" yalifunguliwa na Katibu Tawala Wilaya Bw. John Mahali ambaye aliyekuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo Bw. Mahali alisisitiza kutolewa kwa zawadi mapema iwezekanavyo kwa wafanyakazi bora waliotunukiwa vyeti pamoja na fedha ili kuondoa malalamiko kwa wafanyakazi na kutoa motisha kwa wafanyakzi

Aliwataka wakurugenzi kuweka utaratibu maalumu wa kuandaa vitambulisho vya watumishi ambavyo vitakuwa na Mihuri ya Halmashauri husika na nembo ili kutoruhusu wafanyakazi kujitengenezea wenyewe hali inayopelekea vitambulisho hivyo kukosa viwango na kuonekana ni batili kwa baadhi ya maeneo ambayo wanakuwa wanaonesha kama utambulisho wa mfanyakazi.

Aliongeza kuwa wajibu wa kuandaa nyaraka za watumishi ni za mwajiri ikiwa ni pamoja na barua za ajira, kupanda vyeo na barua za kuthibithishwa, mwajiriwa anawajibu wa kuzitunza Bw. Mahali aliwataka Wakurugenzi kuhakikisha wanatoa nyaraka hizo kwa wafanyakazi wote wenye sifa za kupata nyaraka hizo mapema iwezekanavyo.

" kama kuna Halmashauri ambayo bado haijatoa nyaraka hizo kwa watumishi wao naomba kabisa nyaraka ziandaliwe na kupewa kwa wale ambao hawajapewa, na bahati nzuri mimi ni mtawala na ninaelewa umuhimu wa nyaraka hizo kwa watumishi, Wakurugenzi naomba mtoe nyaraka hizo kwa watumishi" alisema Bw. Mahali.

Kuhusu masuala ya michango alisema kuwepo na utaratibu maalumu ambapo vyama vya wafanyakazi vihusishwe ili kuwe na utaratibu unaoeleweka maana michango mingine ni kwaaajili ya maendeleo yetu sisi wenyewe akitolea mfano wa michango ya mwenge wa uhuru na madawati.

" msikatae kutoa michango ila iwe kwa utaratibu unaoeleweka kwa kupelekwa kwenye vyama vyenu, vyama viridhie kutoa hiyo michango ili kuepuka kuchanga mara mbilimbili hata maeneo mengine ndivyo wanavyofanya" alisema Bw. Mahali.

Ucheleweshaji wa malipo ya mafao Bw. Mahali aliwaeleza wafanayakazi kuwa Halmashauri pamoja na vyama vitaaandika barua ya malalamiko ngazi ya Mkoa ya kucheleweshewa mafao kwa wastaafu ili Serikali ione ni namna gani inaweza kusaidia kutatua changamoto hiyo na kuwataka watumishi wawe wavumilivu.

Mwisho aliwashauri watumishi kutumia ipasavyo bima za afya kwa kuchunguza afya zao mara kwa mara badala ya kusubiri waugue ndipo waende hospitali kwa matibabu. Aliwataka kutilia mkazo suala la mazoezi ya mwili kwani ni kwaajili ya ustawi wa afya zao wenyewe na kinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Maadhimisho hayo yalijumuisha Halmashauri ya Wilaya Handeni na Handeni Mji ambapo viongozi mbalimbali na wafanyakazi walijumuika kwa pamoja.

# Wananchi Wilayani Handeni wahimizwa kuwapeleka watoto kupatiwa chanjo

Wananchi Wilayani Handeni wametakiwa kutilia mkazo suala la kuwapeleka watoto kupata chanjo mara zinapotangazwa ili kuendana na msemo wa kinga ni bora kuliko tiba.

Rai hiyo ilitolewa wakati wa uzinduzi wa wiki ya chanjo ya polio yenye kauli mbiu ya "jamii iliyochanjwa ni jamii yenye afya" uliofanyika katika Zahanati ya Mumbwi iliyopo Katika Kijiji cha Mumbwi kata ya Komkonga.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe mbaye pia alikuwa mgeni rasmi alieleza kuwa Serikali inajitahidi kutoa chanjo bure hivyo wazazi wanao wajibu wa kuhakikisha wanapeleka watoto wao kupata chanjo hizo kwaajili ya ustawi wa afya za watoto.

"Halmashauri ya Wilaya ya Handeni inazo chanjo za kutosha, chanjo mkoba na chanjo tembezi zitafika kwenye maeneo ambayo bado hayana Zahanati ili kuhakikisha watoto wote Wilayani Handeni wanachanjwa" alisema Mh. Gondwe.

Aidha , aliwataka Maafisa Tarafa, Watendaji Kata na Vijiji kuweka agenda ya usafi na mazingira, afya na bima kuwa ndelevu katika vikao vyao vya Vijiji.

Akizungumzia suala la malaria kwenye siku ya maadhimisho ya siku ya malaria duniani Mh. Gondwe alisema kila mwanachi anawajibu wa kutunza mazingira na kutokomeza mazalia ya mbu ili kutokomeza kabisa ugonjwa huo.

"Chanjo zinatolewa bure,vipimo vya malaria vinatolewa bure na baadhi ya dawa za malaria pia lakini ni vyema kila mwananchi kuwa na bima ya afya ili kuepuka gharama za matibabu na kuhakikisha kuwa suala la afya haliwi tatizo kwenye Wilaya ya Handeni"alisema Mh.Gondwe

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Bw. Simon Mdaki alieleza kuwa chanjo zinagharamiwa hivyo ni vyema wazazi kutambua umuhimu wa kupeleka watoto kupata chanjo,mtoto akiugua wasikimbilie imani ya kulogwa badala yake wamuwahishe hospitali ili kufanyiwa uchunguzi wa ugonjwa unaomsumbua. Polio sio ugonjwa wa kulogwa ni chanjo ndio inapaswa kupatiwa mtoto angali akiwa mdogo.

Aidha aliwataka wananchi wote kuzingatia kinga na kutunza mazingira kutokomeza madimbwi na mazalia ya mbu huku wakizingatia matumizi bora ya vyandarua ili kujikinga na ugonjwa wa malaria.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilikuwa na lengo la kutoa chanjo kwa watoto 2883 badala yake wamechanja watoto 3435 sawa na asilimia 119 (kwa kipimo cha penta) mbali na changamoto mbalimbali zinazokabili Idara ya Afya.

Uzinduzi huo ulipambwa na kikundi cha ngoma za asili cha chanika kofi na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali kutoka Halmashauri ya Wilaya wakiwemo Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wa Chama CCM Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Handeni, Wataalamu wa Afya na watendaji wa Halmashauri.



*.Viongozi mbalimbali wakiwa wamebeba watoto mara baada Mkuu wa Wilaya kuwapatia chanjo watoto hao ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa zoezi hilo wa kwanza kulia ni Mh Sophia Sowa Diwani viti maalumu Tarafa ya Mzundu, akifutiwa na Mh. Godwin Gondwe, Mwenyekiti wa chama CCM Handeni Bw.Athumani Malunda, Kaimu Mkurugenzi Bw. Simon Mdaki.*

# Jukwaa la kuwezesha wanawake kiuchumi limezinduliwa Wilayani Handeni

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imezindua jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa wanawake wa Wilaya ya Handeni kwenye ukumbi wa Maount Ilulu uliopo Kabuku lililobeba ujumbe wa “Wezesha wanawake kiuchumi ili kujenga uchumi wa kati na Tanzania ya Viwanda”.

Jukwaa hili linalengo la kuwakutanisha wanawake pamoja na kujadili fursa, changamoto na jinsi ya kushiriki kikamilifu katika biashara na shughuli nyingine za kiuchumi katika Wilaya ya Handeni.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa Jukwaa hilo Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni Bw. John Mahali aliyekuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe alisema kuwa jukwaa la wanawake hilo litasaidia kuongeza uelewa kwa wanawake katika upatikanaji wa mitaji , sheria za nchi katika masuala ya kiuchumi na jinsi ya kujitegemea.

Aliongeza kuwa wanawake wamekuwa hawapati fursa za kutosha za kiuchumi hapa Nchini hata na duniani kote kutokana na kutokuwa na usawa katika fursa na uwezo wa kupata mitaji.

“jukwaaa litasaidia kuondoa matabaka na sheria ambazo zitasaidia kupunguza ubaguzi wa kiuchumi kwa wanawake, ambalo ni jambo la muhimu sana katika kuleta maendeleo ya usawa katika pato la Taifa, jamii na familia” alisema Bw. John.

Kwa upande wake Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe alisema kuwa jukwaa hili litafanya

kutambua shughuli za

Handeni Bw. William Makufwe alisemakuwa jukwaa hili litafanya kazi ya kutambua shughuli za kijasiliamalikatika kutoa elimu kuhusu upatikanaji wa mitaji, kusajili biashara, kuwezesha kiuchumi na kutafuta masoko.

Aidha, alisema katika suala la utoaji mikopo vikundi vitakavyopewa kipaumbele ni vile viliyojidhatiti kwa kusajiliwa, vyenye utawala unaoeleweka, miradi inayoonekana na zenye hesabu za kifedha zinazoweza kukaguliwa na kukosolewa kila inapobidi.

Uzinduzi huo ulipambwa na maonesho ya bidhaa za kijasiliamari ya vikundi mbalimbali kutoka Kata mbalimbali. Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga itaratibu shughuli zote za uchumi kwenye Wilaya zote ndani ya Mkoa na kuhakikisha kunakuwa na majukwaa ya Wilaya/ Halmashauri zote ambayo yatafanya vikao vyake kila baada ya miezi sita (6).



Mkurugenzi Mtendaji Bw. William Makufwe na Katibu tawala Bw. John Mahali wakiangalia moja ya bidhaa kwenye uzinduzi wa jukwaa.

# Mbunge Handeni Vijijini afanya ziara ya kutembelea miradi ya maendeleo

Mbunge wa Handeni vijijini Mh. Mboni Mhita na kamati ya mfuko wa jimbo wametembelea miradi ya mfuko wa jimbo yenye lengo la kuchochea maendeleo.

Katika ziara hiyo Mbunge alilenga kukagua miradi ambayo ilifadhiliwa na fedha za Mfuko wa Jimbo kuona namna gani utekelezaji umefanyika lakini pia kupitia miradi ambayo imeombewa msaada wa kumaliziwa kwa kutumia fedha za mfuko wa jimbo ili kujiridhisha na miradi yenyewe iliyofanywa kwa nguvu za wananchi.

Mbunge pamoja na kamati walipongeza baadhi ya miradi na kupongeza jitihada za wananchi katika kujikwamua na chanagamoto wanazokutana nazo.

Aliwaeleza wananchi na viongozi kuwa Kata inayofanya vizuri ndiyo itakayopewa kipaumbele katika kuletewa miradi na kusaidiwa kumalizia miradi yao.



Darasa lia Mazingra sekondari lililokarabatiwa na mfuko wa jimbo.

# Halmashauri ya Wilaya ya Handeni yakabiliana na upungufu wa dawa kwa kufungua stoo ya dawa iliyopo katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imefungua duka/ stoo ya kuhifadhia dawa ili kukabiliana na changamoto ya upungufu na ukosefu wa dawa kwa wakati kwenye Hospitali ya Wilaya ya Handeni.

Uwepo wa duka hilo umekuja kufuatia changamoto zilizokuwa zinaikabili Hospitali pamoja na Vituo vya Afya ya upungufu na ukosekanaji wa dawa na wakati mwingine kutokupata dawa kwa wakati wanapoagiza Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Akizungumza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni BW. William Makufwe wakati wa ziara ya madiwani kwenye Duka/ Stoo hiyo alisema kuwa, tumeamua kukabiliana na changamoto ya upungufu na malalamiko ya wananchi ya ukosefu wa dawa kwa muda mrefu kwenye Hospitali yetu na vituo vya afya kwa kufungua Duka/Stoo ambayo itakuwa na dawa za aina mbalimbali ili kuboresha huduma.

Aliongeza kuwa vituo vyote vya afya kwasasa vitakuwa vinachukua dawa kwenye duka/stoo ya Hospitali ya Wilaya pindi dawa zinapohitajika badala ya kuagiza moja kwa moja MSD.

Kuagiza dawa MSD kulikuwa kunachelewesha upatikanaji wa dawa kwa wakati na hivyo kusababisha upungufu wa dawa ambao ulikuwa unasababisha malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi.




Waheshimiwa Madiwani na watalaamu mbalimbali wakiingia kutazama dawa zilizopo kwenye stoo hiyo.

"ukiona unapata maelezo yasiyoeleweka kuhusiana na upatikanaji wa dawa kwenye maeneo yote yanayotoa huduma za afya piga simu kwangu moja kwa moja namimi nitashughulikia" alisema Makufwe.

Aidha, aliwaomba waheshimiwa madiwani kuendelea kuhamasisha kaya kuendelea kujiunga na mfuko wa afya wa jamii (CHF) ambao kwa kiasi kikubwa umesaidia upatikanaji wa fedha za kununulia dawa, ambapo kwa kuongeza idadi ya kaya wanaojiunga na CHF kutasaidia kuwepo kwa dawa maratatu zaidi ya zilizopo.

Aliwaomba pia kusimamia dawa zinazopelekwa kwenye vituo vyao vya afya ili kuepuka dawa kuhujumiwa.

Mfamasia wa Hospitali ya Wilaya ya Handeni Mustafa Lutavi alisema kuwa kabla ya kufunguliwa kwa duka hilo hospitali ilikuwa inachangamoto kubwa ya ukosefu wa dawa za kutosha hali iliyopelekea malalamiko ya mara kwa mara ya wananchi wanaopata huduma kwenye hospitali hiyo na vituo vya afya.

Alieleza kuwa CHF imepanga kuboresha huduma zake ambapo badala ya wanachama kupata huduma kwenye vituo vilivyopo Wilayani, wataanza kupata huduma ngazi ya Mkoa. Mbunge wa Handeni Vijijini Mh. Mboni Mhita na waheshimiwa madiwani walimpongeza Mkurugenzi na timu yake nzima kwa ujumla kwa jitihada walizozionesha katika kukabiliana na changamoto hiyo na kwamba wao kama viongozi wenye dhamana kwa wananchi wataendele kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko wa afya wa jamii CHF ili kuendelea kuboresha huduma za Afya, huku akiahidi kuendelea kufuatilia upatikanaji wa watumishi wa idara ya afya kupunguza changamoto ya upungufu wa watumishi.



Baadhi ya Dawa

## Madiwani na wakuu wa Idara na Vitengo wamepatiwa semina ya uelewa wa pamoja kuhusu Matumizi ya fedha za Ruzuku LGDG

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imefanya semina ya Uelewa wa fedha za ruzuku ya maendeleo iliyoboreshwa (LGDG) na mfumo wa Fursa na Vikwazo ulioboreshwa (IMPROVED O&OD) kwa Waheshimiwa Madiwani na Wakuu wa Idara na Vitengo.

Semina hiyo iliyoendeshwa na wataalamu wa Ofisi ya Rais- TAMISEMI na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ililenga kuwajengea uelewa wa pamoja kuhusu fedha za ruzuku ya maendeleo iliyoboreshwa katika maeneo ya:-.

1.Maana na umuhimu wa LGDG
2.Matokeo ya LGDG iliyoboreshwa
3.Changamoto za LGDG iliyopita
4.Vigezo 9 vya kiutendaji na vigezo vya msingi
5.Mgawanyo wa fedha za LGDG
6.Matumizi ya fedha za LGDG

Kwa upande wa ugatuaji wa madaraka (D by D), umuhimu wa mfumo wa fursa na vikwazo ulioboreshwa katika maeneo ya:-

1.Maana ya mpango wa fursa na vikwazo ulioboreshwa (O&OD)
2.Maana ya jitihada za jamii na aina zake
3.Mantiki ya Halmashauri kusaidia jitihada za jamii kwa kuangalia Uhalisia wa Tanzania ndani ya Serikali za Mitaa na Faida za kutoa usaidizi kwa jitihada za jamii.
4.Vigezo vya kuchambua jitihada za jamii
5.Aina za usaidizi wa jitihada za jamii
6.Mifano halisi ya jitihada za zamii kwa video.

Akifungua semina hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe alipongeza ushirikishaji wananchi kutoka ngazi za chini ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wakati na miradi ya maendeleo iliyokamilika kwa kuwepo na nia ya dhati kutoka kwa wananchi




Waheshimiwa Madiwani na Watalaalamu wakisikiliza kwa makini maada za semina kwenye ukumbi wa Halmashauri.

## Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ameshukuru msaada wa kompyuta mbili zilizotolewa na BAYPORT

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw,William Makufwe ameishukuru Taasisi ya kifedha ya BAY PORTkwa msaada wa kompyuta mbili walizozitoa kwa Idara ya Utumishi na Rasilimali watu.

Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa amepokea msaada wa kumpyuta mbili ambazo zitakwenda kwenye Idara ya Utumishi na Rasilimali watu ili kuimarisha Idara na kuongeza ufanisi wa Idara hiyo kwa kuzingatia unyeti wa eneo hilo na huduma wanayoitoa kwa watumishi.

Miongoni mwa Halmashauri 80 ambazo zimelenga kufikiwa na BAYPORT tunashukuru Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imekuwa moja wapo na tunaahidi kutumia vifaa hivi vya TEHAMA kwa kuongeza ufanisi na utendaji kazi ulioboreka zaidi.

Mratibu wa masoko na mawasiliano wa huduma za kifedha za BAYPORT Mercy Ndunguru alisema kuwa BAYPORT imeamua kurudisha faida ambayo wameipata ambapo kwa sasa wameona waguse sekta ya utumishi ambayo imekuwa na msaada mkubwa katika kufikia malengo.

Mercy alisema kuwa, Tunaamini kwa kutoa vifaa hivi vya TEHAMA itasaidia kuongeza ufanisi kwenye sekta ya utumishi na watumishi watapata huduma kwa wakati, BAYPORT inamuunga mkono Raisi kwenye utendaji kazi kwa watumishi.




Afisa Utumishi(W) akipokea msaada wa kompyuta

## Shule 11 zapongezwa kwenye kilele cha juma la Elimu kwa ufaulu mzuri wa mitihani ya mwaka 2016

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imepongeza na kutoa zawadi kwa shule 10 za Msingi na Sekondari 1 kwa kufanya vizuri kwenye mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne mwaka 2016.

Zawadi hizo zilitolewa kwenye kilele cha maadhimisho ya juma la elimu yaliyofanyika kiwilaya kwenye shule ya Msingi Kabuku nje.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo Mkuu wa Wilaya ya Handeni ambaye pia alikuwa mgeni rasmi Mh. Godwin Gondwe aliwapongeza walimu na wadau wengine wa elimu kwa kazi nzuri wanazofanya na wanazoendelea kufanya katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora.
*"elimu ni ufunguo wa maisha na kwamba Handeni hakuna mtoto mjinga, wazazi na walezi himizeni watoto kutumia fursa ya Elimu bure inayotolewa na Raisi wa Tanzania"* Alisema.

Aidha alieleza kuwa atahakikisha fedha zinazohusu madai ya walimu zinapofika Halmashauri zinawafikie walengwa kwa wakati uliopangwa. Aliwataka wakuu wa shule na Maafisa elimu Kata kusimamia haki ya msingi ya wanafunzi kupata elimu wanayostahili.

Wakati huohuo amepiga marufuku watoto walio na umri wa kuwepo shuleni kuacha kuchunga mifugo hasa kwa siku za shule baada ya kubainika watoto wengi wa jamii ya wafugaji wanatumiwa kuchunga mifugo badala ya kwenda shule.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chogo Bi.Sifael Mchalo akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe

Amewaonya wazazi na jamii ya wafugaji ambao wanakwamisha watoto kupata haki yao ya msingi ya kupata elimu kwamba sheria itachukua mkondo wake kwa yeyote atakayebainika kwenda kinyume. Amewaeleza pia wazazi ambao wanawatoto waliovuka umri wa kwenda shule kupelekwa kwa utaratibu wa MEMKWA.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Bw. William Makufwe ,amesema kuwa kukosekana kwa chakula cha kutosha shuleni,utoro uliokithiri kwa baadhi ya wanafunzi,kutokuwajibika kwa baadhi ya walimu na wazazi pamoja na upungufu wa walimu kunasababisha kwa kiwango kikubwa kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi.

Aliagiza shule ambazo hazina chakula kuhakikisha wanawapa wanafunzi chakula. Aliwataka pia kusimamia mazao ya mihogo waliyopanda ili mazao hayo yaweze kusaidia upatikanaji wa chakula shuleni na kuongeza kiwango cha uelewa kwa wanafunzi.

Ametoa mwezi mmoja hadi kufikia 4/5/20167kwa Maafisa watendaji Kata, Vijiji, walimu wakuu, wakuu wa shule na Maafisa elimu Kata kuhakikisha kuwa watoto wanapata chakula cha mchana shuleni.

Shule za Msingi zilizopata zawadi na pongezi ni Tewe iliyokuwa ya sita kimkoa na kuzawadiwa Tsh. 200,000/=., Chang'ombe Tsh. 150,000/=, Mkumba Tsh 100,000/=, Mzundu Tsh. 82,000/=, Kwaragulu , Mbwewe, Kwamdani, Kwedikwazu Magharibi, Kwedikwazu Mashariki na chogo ambazo zote zilipata Tsh 78,000/=. Mazingara sekondari imepata zawadi Tsh.100000/=.



Mkuu wa Wilaya Mh. Godwin Gondwe akizungumza na wanafunzi

## Baraza la madiwani limepongeza miradi ya ajira za muda mfupi zilizofanywa na wanufaika wa Mfuko wa kunusuru kaya masikini TASAF

Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Handeni limepongeza utekelezaji wa mradi wa ajira za muda mfupi za uchimbaji wa malambo ya maji wa TASAF, Miradi ambayo imechimbwa na wanufaika wa mfuko wa kunusuru kaya masikini (TASAF) kuvuna maji katika kipindi cha mvua.

Pongezi hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki kwenye Baraza la madiwani lililofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Akizungumza , Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Ramadhani Diliwa alisema kuwa wamepitia miradi ya malambo yote na kuona namna ambavyo wananchi wamejitoa kuchimba kwa ufanisi mkubwa malambo hayo mbali na kwamba, kipindi cha utekelezaji kulikua na changamoto ya jua kali na uhaba wa chakula.

*"Malambo yamechimbwa kwa mikono na walengwa lakini ukiyaangalia utadhani ni mashine ndio imechimba, Hongereni sana"* alisema Mwenyekiti

Aliongeza kuwa kutokana na changamoto ya kuwepo na maji ya uhakika,wananchi watakuwa na uhakika wa maji kutokana na malambo hayo na hivyo kuwataka kuhakikisha wanayatunza ili yawasaidie hasa katika kipindi ambacho mvua itakuwa imekata

Aidha, alieleza kuwa kuhusiana na changamoto ya malipo kwa walengwa waliofanya kazi hizo kuwa wavumilivu kwa kipindi hiki ambacho fedha zao zinashughulikiwa na mara fedha zitakapowasilishwa Halmashauri itahakikisha inawalipa kwa wakati.

Jumla ya Malambo 63 yamechimbwa ambapo vijiji 45 vinatarajiwa kunufaika na mradi wa malambo hayo katika kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa maji ya uhakika.Mradi wa kunusuru kaya masikini TASAF umeibua miradi ya barabara 4, visima 17 na malambo 63 ambapo miradi yote imegharimu jumla ya Tsh. 661,622,600/=.



Rambo lililopo katika kijiji cha Kwabojo.

## Watumishi 5 waliokuwa wanakaimu Idara na Vitengo wamethibitishwa na Baraza la Madiwani .

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Handeni limeridhia na kuwapitisha watumishi watano kuwa wakuu wa Idara na Vitengo baada ya kuridhishwa na utendaji wao wa kazi.

Ridhaa hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Handeni, Ramadhani Diliwa katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya wilaya Handeni hivi karibuni.

Diliwa alisema kuwa Baraza lake limetathmini kazi za watumishi hao watano na kuridhishwa na utendaji wao wa kazi na kufikia maamuzi ya kuwapitisha kuwa wakuu wa Idara na Vitengo. Aliwataja watumishi hao na nafasi zao katika mabano kuwa ni Mosses Chilla (Mkuu wa Idara ya Takwimu, Mipango na Ufuatiliaji), Fikeni Senzighe (Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi), Julius Omary (Mkuu wa Idara ya Ujenzi na zimamoto), Saturine Kessy (Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani) na Mussa Kimwaga (Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi). Aidha, Napoleone Mlowe aliidhinishwa kuwa Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili.

"Fanyeni kazi kwa weledi kuonesha Baraza halijakosea"alisema Diliwa.

# Wananchi Wilayani Handeni wapigwa marufuku kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji.

Wananchi wilayani Handeni wapigwa marufuku kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka katika vyanzo vya maji na kutakiwa kutunza mazingira ili kuwezesha uendelevu wa maisha.

Marufuku hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Handeni,Mh.Godwin Gondwe aliyekuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira duniani yaliyofanyika ngazi ya wilaya Kata ya Mkata katika bwawa la Tulafimbo.

Gondwe alisema kuwa wananchi lazima wazingatie sheria ya Mazingira inayozuia kufanya shughuli za kibinadamu pamoja na kujenga kwenye maeneo yote ya vyanzo vya maji ndani ya mita 60.

"Kwa kuzingatia sheria hiyo, kupiga marufuku kwa wananchi kufanya shughuli zozote za kibinadamu zenye kuhatarisha usalama wa maji na uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo yanayozunguka vyanzo vya maji wilayani Handeni" alisema Gondwe.

Aidha, aliwataka maafisa Tarafa, maafisa watendaji wa Kata na wenyeviti wa Vijiji kuhakikisha wanatengeneza mipaka kwenye maeneo ya vyanzo vya maji vyote vilivyopo Wilayani Handeni msimu huu ambao mvua imenyesha ya kutosha na vyanzo vingi vimejaa maji. "Hii itasaidia kuzuia uvamizi wa maeneo hayo na kurahisisha kuchukua hatua kwa watu watakaokwenda kinyume na amri hiyo" alisema Gondwe.

Gondwe, aliwataka wananchi wote walionunua mashamba kwa lengo la kilimo kusafisha mashamba yao kwa kuacha asilimia 30 ya uoto wa asili badala ya kusafisha maeneo yote ambayo wamenunua. "Tusipotunza mazingira, itakuwa ni ubinafsi kwa kizazi chetu na kizazi kijacho. Tukitendee haki kizazi hiki na kijacho kwa kuondoa ubinafsi wa kuharibu mazingira" alisema Gondwe.

Wakati huohuo, aliwataka viongozi ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji kutunza mazingira kwa kusimamia uwiano wa ardhi uliyopo na idadi ya mifugo ili kutunza mazingira kwa kuwa na mifugo inayoendana na rasilimali ardhi iliyopo. Aliwataka kuweka mikakati ya kupiga chapa mifugo ili kurahisisha utambuzi wa mifugo hiyo wilayani Handeni.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, William Makufwe aliwataka wananchi kutunza rasilimali maji kidogo inayopatikana kwa kipindi cha mvua, kwa kupanda miti kwenye maeneo yanayozunguka vyanzo vya maji. Alisema kuwa Serikali inaendelea kushughulikia changamoto ya upatikanaji maji ya kudumu Wilayani Handeni.

Aliwataka wakuu wa shule za msingi na sekondari kuhakikisha kila mwanafunzi anayeanza darasa la kwanza hadi la saba na kidato cha kwanza hadi cha nne anakuwa na mti wake anaoutunza ili anapomaliza shule akikabidhiwa cheti na yeye akabidhi mti alioutunza kwa kipindi chote alichokuwa shuleni.

Maadhimisho ya wiki ya mazingira kiwilaya yalitanguliwa na upandaji miti 28,954 yakiongozwa na kaulimbiu isemayo "hifadhi ya mazingira muhimili kwa Tanzania ya viwanda".



Mkurugenzi Mtendaji Bw. William Makufwe aliyeshika chepeo akimsaidia Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Ramadhani Diliwa kufukia vizuri mche wa mti mara baada ya kupandwa ikiwa ni ishara ya maadhimisho hayo.

## Halmashauri ya Wilaya ya Handeni yapokea Miche ya mbegu za Korosho 4000 zitakazopandwa kwenye taasisi za shule

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imepokea miche 4000 ya mbegu za korosho kutoka bodi ya korosho ili kuunga mkono juhudi za Serikali ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ya kuanzisha korosho kama zao la biashara.

Miche hiyo ya mbegu za Mikorosho zilipokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe na kukabidhiwa kwa Maafisa Elimu tayari kupelekwa kwenye Shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya kupandwa.

Akizungumza na Maafisa Ugani, Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari na Maafisa Kilimo Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Gondwe alieleza kuwa, kwa muda mrefu Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imekuwa haina zao la biashara la uhakika na wakati huohuo kuna ukanda ambao kunastawi zao la korosho, hivyo ni muhimu kuchukulia zao hili kama zao la biashara bila kujali ni muda gani unachukua mpaka mavuno.

"korosho linakuwa ni zao la biashara Wilayani Handeni, ni mti ambao utasaidia kutunza mazingira pia, lengo ni kuongeza uchumi wa wananchi, kushirikisha wanafunzi kwenye elimu ya kujitegemea na kuhakikisha wanafunzi hawapati shida ya chakula hatimaye kuongeza kiwango cha uelewa na ufaulu kwa watoto wetu" alisema Mh. Gondwe.

Mh.Gondwe Aliongeza kuwa mbegu hizi zitasambazwa kwenye taasisi za elimu hasa kwa shule ambazo zipo ukanda wa Korosho na hazikupata mbegu za mihogo au zilipata kwa kiwango kidogo, ili iwe rahisi kusimamia na kufanya mashamba darasa kwa jamii inayozunguka shule.

Mh. Gondwe Aliwataka Maafisa kilimo kuwaandikia barua zitakazowataka kusimamia na kutoa elimu ya kilimo bora cha zao la mikorosho maafisa ugani wote watakaohusika na upokeaji wa mbegu kwenye maeneo yao.

Kuhusu suala la masoko Mh. Gondwe aliwatoa hofu na kuwaeleza kuwa masoko ya korosho Tanzania yapo na bado ataendelea kutafuta masoko huku akiwaasa katika suala la uvunaji bora ambao utaanzia kwenye matunzo ya zao tangu kupandwa hadi kuvunwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Mh. Ramadhani Diliwa aliwaeleza wataalamu kuwa wananchi wa Wilaya ya Handeni hawajachelewa kuanza zao hilo.

kulima mazao mengine ya biashara huku akisisitiza upandaji wa miti ambao kwa wakati mwingine ni kutunza mazingira na kwa upande mwingine ni biashara.

*" Tuache kushikilia zao la mahindi kama zao kuu la Handeni, wananchi amkeni, limeni mazao mengine ardhi ya Handeni inarutuba ya kutosha na uwezo wa kustawi mazao mengine zaidi ya mahindi, mimi nina ekari zaidi ya 50 ambazo nimelima mazao mbalimbali na kupanda miti aina tofauti karibuni mje kujifunza "* alisema mwenyekiti.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Bw. Simon Mdaki alishukuru kupokea mbegu hizo na kuwataka Maafisa Kilimo, Wakuu wa Shule kusimamia ukuaji wa zao hilo kwa weledi ili kuweza kufikia lengo la Halmashauri ya Wilaya ya Handeni katika kuondoa dhana potofu ya wananchi wa Wilaya ya Handeni kutegemea zao moja tu la mahindi.



Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe akikabidhi mbegu za Korosho kwa Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari Bw. Simon Mdaki

# Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imepongeza jamii za wamasai waliokubali kuvusha rika watoto wa kike bila kuwakeketa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kwanza Kushoto akifuatiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Ramadhani Diliwa na viongozi wa kimasai walipokuwa wakikaribishwa kwenye sherehe za uvushaji rika Kijiji cha Msomera

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na Mkurugenzi Mtendaji wameshiriki sherehe za uvushaji rika kwa wasichana wa jamii ya kimasai bila kukeketwa baada ya kupatiwaa elimu kutoka shirika lisilo la kiserikli la Amref juu ya madhara ya ukeketaji kwa watoto wa kike na wanawake walio na umri wa kujifungua.

Mwenyekiti wa Halmashauri amepongeza Leigwanan, mangariba na jamii nzima ya wamasai waliokubali kubadili mila iliyokuwa inawakandamiza watoto wa kike kwa kuwakeketa.

Akizungumza kwenye sherehe hizo amesema kuwa Amref wameunga mkono Serikali kwenye kupambana na vitendo vya ukeketaji kwa wasichana kwa kuwapatia elimu ya ufahamu na kutumia njia mbadala ya kuwavusha wasichana hao bila kuharibu tamaduni zao.

“Serikali haitakuwa tayari kumvumilia mtu yeyote atakayeendeleza vitendo vya ukeketaji kwa watoto wa kike hasa mara baada ya elimu hii kutolewa, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake”alisema Diliwa.

Mkurugenzi mtendaji Bw. William Makufwe alipongeza jitihada za Amref na kuahidi kuziendeleza hata mara baada ya mradi huo kukoma.

Meneja wa mradi Dk.Sarafina Mkuwa amesema kuwa katika kipindi cha miezi sita mradi umeweza kuwajengea uwezo wasichana 540 kutambua haki zao,wanawake 270, ngariba 50,morani 108 na viongozi wa kimila zaidi ya 100 ambao wamepatiwa elimu ya afya na madhara ya ukeketaji.

Mradi wa ELIMISHA ulianza Januari 2017 na unatarajiwa kuisha Desemba 2017 ambapo jumla ya Kata 5 za Wilaya ya Handeni zitafikiwa .Wavushwaji rika wameweza kupata mafunzo ya madhara ya ukeketaji,stadi za maisha,mbinu za kufanya maamuzi kwa wakati sahihi, mzunguko wa hedhi, magonjwa ya ngono na mila za kimasai ambazo sio potofu.




Viongozi mbalimbali ngazi ya Halmashauri wakiongozwa na mwenyekiti wa Halmasahuri katika picha ya pamoja na baadhi ya watoto wa kike waliovushwa rika bila kukeketwa wakiwa wameshika vyeti kuashiria hakuna tena ukeketaji.

# Mkuu wa Mkoa wa Tanga ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kufuata Sheria za manunuzi ili kuepuka hoja zinazoweza kuzuilika.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mh. Martin Shigella ameipongeza Halmashauri ya Wiaya ya Handeni kwa kuwa na hati safi na kuwataka kufuata kanuni za manunuzi na kuweka kumbukumbu sahihi ili kuepuka kutengeneza hoja zinazoweza kuzuilika.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mh. Martine Shigella akizungumza wakati wa kikao cha hoja za CAG katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya yaHandeni

Ameyazungumza hayo alipokuwa kwenye kikao cha Baraza la Hoja za CAG kilichofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Mkuu wa Mkoa amesema kuwa manunuzi yote yanayaofanyika yanapaswa kuwa na vielelezo halali ili kuepuka kutengeneza hoja ambazo zingeweza kufutika, hoja ya kukosekana kwa vielelezo Halmashauri ichukue hatua kwa watendaji watakaohusika ambao wanatumia mianya kujinufaisha wenyewe.

Ameongeza kuwa fedha zinazoletwa ni muhimu zikatumika kwa wakati kwani mahitaji ya wananchi ni mengi na makubwa ili kuepuka bakaa, zibaki fedha ambazo hazikuletwa kwa wakati hivyo kuchelewesha matumizi yake, fedha ambazo kwa wakati huo ndio Halmashauri imetangaza zabuni na sio sababu ya kushindwa kutumika.

“wekeni utaratibu wa kuhakikisha kila vikao mnavyokaa hususani kamati ya fedha mnajadili kiasi cha fedha kilichopo kwenye kila akaunti ili kujua matumizi yake kuepuka bakaa zinazoweza kuzuilika,Wananchi wanahitaji kuhudumiwa kwa fedha hizo zinazoletwa na Serikali” Amesema Shigella.

Amesema kuwa hoja za malipo kwa watumishi hewa zisijirudie kwa kuhakikisha watumishi wote wanaokuja wanahakikiwa na kulipwa fedha kwa uhalali.

Kwa upande mwingine Katibu Tawala Mkoa Bi. Zena Said amesema kuwa fedha za mifuko ya afya CHF na NHIF hazitakiwi kupita mwaka labda ziwe zimechelewa kuletwa.

Madai ya watumishi kutokuwa na uhalisia ameishauri Halmashauri kuhakikisha madai ambayo watumishi wanayadai kwa Serikali kuwa yamethibitishwa uhalali wake na kuonesha ushaidi na kuondoa dhana ya kufikiri Serikali inafedha nyingi kwaajili ya malipo hayo.

Mwenyekiti wa Wilaya ya Handeni Mh. Ramadhani Diliwa ameshukuru Mkuu wa Mkoa na timu nzima kutoka Mkoani kwa kushiriki pamoja na Halmashuri na kuahidi kusimamia utekelezaji maagizo yote yaliyotolewa kuepuka hoja zinazoweza kuepukika.



Mkaguzi wa Ndani Bw. Saturine Kessy akiwasilisha Hoja wakati wa kikao cha hoja za ukaguzi CAG.

## HABARI KATIKA PICHA



Mbunge wa Handeni Vijijini Mh. Mboni Mhita akikagua mihogo alipokuwa kwenye ziara ya ukaguzi wa miradi .



Mbunge wa Handeni Vijijini Mh. Mboni Mhita akizungumza na wananchi wa Kwamsisi.



Mkuu wa Wilaya ya Handeni akimpatia mtoto matone ya chanjo kwenye ufunguzi wa zoezi la utoaji chanjo.



Afisa Elimu Msingi Wilaya Bw. Fikeni Senzighe akikabidhi mbegu ya korosho  kwa mkuu wa shule.



Vikundi mbalimbali vya bidhaa za kinamama vilivyojitokeza kwenye uzinduzi wa Jukwaa la kuwezesha wanawake kiuchumi uliofanyika  Kabuku.




Picha ya pamoja ya Waheshimiwa Madiwani na wataalamu wa Halmashauri walipotembelea stoo ya Dawa iliyopo Hospitali ya Wilaya.

# HABARI KATIKA PICHA



Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe akipanda Mti kwenye kilele cha siku ya mazingira akisaidiwa na Afisa mazingira Wilaya aliyeshika chepeo Bw. Leonard Mkayula.



Wanafunzi wa shule ya sekondari Kabuku wakionesha uwezo wao kwenye somo la fizikia (mafunzo kwa vitendo) kwa viongozi kwenye kilele cha juma la Elimu lililofanyika Kabuku.



Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za jamii Mh. Joel Mabula akizungumza na wananfunzi wanaojiandaa na UMITASHUMTA kwenye kambi ya Kabuku.



Meneja wa Mradi wa STOP FGM kutoka Amref Dk Sarah Mukua wa kwanza kushoto akifafanua jambo kwa viongozi na jamii nzima ya wamasai.



Msafara wa Viongozi kuelekea Hospitali ya Wilaya kushuhudia stoo ya dawa iliyofunguliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kupunguza changamoto ya dawa




Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mh. Martine Shigela katikati akipongeza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kwa ufunguzi wa Stoo ya Dawa.